TANGAZO LA SERIKALI Na. 50M la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

## AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO ITOKANAYO NA HUDUMA YA KIHANDISI NA HUDUMA ZA UJENZI KATIKA MRADI WA UANZISHWAJI NA UENDESHAJI WA MTAMBO WA UKOBOAJI NA UFUNGASHAJI MCHELE KWA KAMPUNI YA WILMAR RICE TANZANIA LIMITED YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye huduma ya kihandisi na Huduma ya ujenzi katika Uanzishwaji na Uendeshaji wa Mtambo wa Ukoboaji na Ufungashaji wa Mchele wa Kampuni ya Wilmar Rice Tanzania Limited ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 3 Julai, 2024

Msamaha

**2.** Kodi ya Zuio kwenye huduma ya kihandisi na Huduma ya ujenzi zinazopaswa kulipwa na Kampuni ya Wilmar Rice Tanzania Limited katika utekelezaji wa Mradi wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Mtambo wa Ukoboaji na Ufungashaji wa Mchele inasamehewa.

Ukomo

**3.** Amri hii itafika ukomo wake tarehe 31 Mei, 2026 kwa mujibu wa kipengele cha 3.3 cha Mkataba wa Utekelezaji ulioingiwa baina ya kampuni ya Wilmar Rice Tanzania Limited na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliosainiwa tarehe 23 Juni, 2023.

Dodoma,
31 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*